**African Entrepreneurs – Successful and Responsible**

**Episode 4**

**Title: “Swimming against the current – Giordano Custódio from Cape Verde”**

**Author: Nélio dos Santos / Johannes Beck**

**Editors: Katrin Ogunsade / Adrian Kriesch**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters (O-Töne/clips) / Narrators**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | x | | Unimportant | |
| Narrator | | X | Unimportant | |
| Giordano Custódio (clip) | | X | about 40 | Portuguese |
| Edson Custódio (clip) | | X | about 25 | Portuguese |
| Pedro Moreira (clip) | | X | about 40 | Portuguese |

**<u>Pronounciation [as it would be in english]:</u>**

Giordano Custódio [Jor-d'a-no Kuch-t'o-di-yu]

GC Comunicações [Ge Ci Ko-mu-ni-ka-s'ois]

Praia [Pr'a-ya]

Crioulo [Kri-'o-lu]

Pedro Moreira [P'e-dru Mo-r'ey-ra]

Rádiu Kultura [R'a-diu Kul-tu-ra]

Nélio dos Santos [N'e-liu duch S'an-tuch]

**Intro:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine kwenye mfululizo wa vipindi vya Learning By Ear, Noa Bongo Jenga Maisha yako.Bado tuko kwenye masuala ya uwekezaji ambapo tunawaangazia wajarisimali chipukizi Barani Africa, ambao ufanisi wao umesaidia kubadilisha maisha ya wengi miongoni mwa jamii wanaoishi.Safari yetu inatupeleka hadi kisiwa cha Cape Verde , Africa Magharibi ambako tunakutana na mfanyi biashara mashuhuri katika sekta ya habari na mawasiliano.

**1. Giordano Custódio:**

"Jina langu ni Giordano Custódio. Mimi ni mtaalam wa saikolojia na nina umri wa miak 46.Nafanya biashara Katika sekta ya mawasiliano.
Mimi ndie mkurugenzi wa shirika la mawasiliano la GC comunicacoe na pia kuwa miongoni mwa washikadau wakuu katika kampuni hii.Napenda sana muziki .

**2. SFX Promotional Spot:**

**3. Narrator:**

Ni kupitia vipindi vya matangazo ya kibiashara ambapo Vyuombo vya habari vimeweza kujenga msingi bora na kukuza shughuli za uzambazaji habari mbali na ushawishi mkubwa mjini Cape Verde .

Mnamo mwaka wa 1997,Giordano custodio aliwacha kazi katika shirika la kitaifa la redio na televisheni,na kuanzisha biashra yake binafsi .Pamoja na kaka zake wawili aliweza kuanzisha kampuni ya matangazo ya GC comunicacoes.

Giordano aliweza kuanzisha kampuni hii ya matangazo kwa kutumia marupurupu na Mkopo wa benki uliofika mtaji wa kima cha cha Euro 10,000, Na kufikia sasa kampuni hiyo ya GC comunicacoes, imeweza kutayarisha matangazo elfu mbili ya biashara kila mwaka yanayopeperushwa hewani na vituo mbali mbali vya redio kote nchini Cape verde,ikiwa ni pamoja na mashirika maarufu yanayoongoza katika fani hiyo nchini humo .

Azma ubunifu,maono na bidii imekuwa nguzo muhimu katika ufanisi wa Giordano Custordio. Mbali na hayo familia yake pia imechangia pakubwa ufanisi huu. Edson Custodio mwanawe wa kwanza wa kiume anapendwa sana na Babake na amekuwa msaidizi wa karibu katika shughuli hii.

**4. Edson Custódio:**

“Kama mkurugenzi wa kampuni hii ya GC Comunicações Babangu ana kipawa na ujuzi wa hali ya juu na ni Mtu anayefahamu kila anachofanya. Ukweli ni kwamba yeye ni mtaalam katika sekta hii ya mawasiliano na ni mfano bora wa kuigwa.Mbali na kwamba yeye ni mtaalam wa saikolojia ya mawasiliano, pia ni mtu mbunifu sana, ni rahisi sana kumwelezea Babangu Kwa ufipi yeye ni kama rafiki yangu mkubwa”.

**5. Narrator:**

Baada ya kuanzisha kampuni ya matangazo mwaka wa 1997 , haikumchukua muda kabla ya Giordano Custódio kujitosa katika fani nyingine . Mnamo tarehe $15^{t}$ mwezi Machi 1999 aliweza kufungua kituo cha redio cha Praia FM na kuanza kupeperusha matangao yake. Kituo hicho cha redio kilichoko ufuoni mwa bahari kilipindukia kuwa maarufu sana katika mji mkuu Praia nchini Cape Verde. Na hadi sasa bado ni maarufu sana miongoni mwa vituo vinavyopeperusha matangazo katika mji huo mkuu wenye idadi ya watu wapatao 125.000.

**6. SFX Praia FM:**

**7. Narrator:**

"Muziki huwavutia vijana wengi sana na watangazaji wa kituo hiki wanaotangaza kwa lugha ya Crioulo,inayozungumza na raia wengi wa Cape Verde, japo lugha rasmi ya nchi hiyo ni Kireno, wamekuwa kivutio kikubwa na kuongeza umaarufu wa kituo hicho cha Praia, mbali na shughuli za kawaida za kampuni ya mawasiliano ya GC Comunicações".

Pedro Moreira ni mwandishi wa habari na afisa wa ngazi za juu katika kampuni hiyo ya GC Comunicações. Amekuwa akifanya kazi katika kampuni hii tangu kituo cha utangzaji cha Praia kilipoanza kupeperusha matangazo yake. Giordano Custódio pia anampenda sana mfanyi kazi huyu na amekuwa rafikiye mkubwa.

**8. Pedro Moreira:**

Giordano Custódio sio tu ni mkubwa wangu kazini,ni namchukulia tu kama mfanyikazi mwenzangu,mkurugenzi ambaye hakosekani kazini,na ambaye anajali maslahi ya wafanyikazi. Hii yote ikiwa ni katika juhudi za kubuni mazingira bora kazini. Kwa ufupi ni yeye ni mfanyakazi mwenzangu tu.

**9. SFX Jingle Praia FM:**

**10. Narrator:**

Wakati kituo cha Praia kilipokuwa kikiendelea kuimarika. Giordano Custódio alianzisha mradi mwengine mwaka wa 2010. Alifungua kituo cha pili cha Redio kwa jina Praia fm2 –radiu kultura.

**11. SFX Rádiu Kultura:**

**12. Giordano Custódio:**

Tuligundua kwamba vituo vingi vya Redio vinavyohudumu Cape Verde vilianza kuiga mpangilio na ratiba ya matangazo yetu. Hivyo vituo vingi vikaanzishwa kwa jina la Praia FM, mfano Paia FM 1, 2,3,4,5,6 na kadhalika, Hata shirika la taifa la utangazaji pia liliiga mfano wetu na kuanzisha kituo cha Praia FM, Na tulitaka kuwa tofauti, kwamba unaweza kuanzisha kituo pasi na kuiga mfano wa mwengine, ndio tukanzisha kituo hiki cha Rádiu Kultura. Hata hivyo si rahisi kusimamia kituo cha utamaduni na kinachofuata mpangilio wa aina hii, Hata hivyo kiimeanza kuimarika pole pole hasa tukizingatia uwezo wetu na mambo yanavyokwenda."

**13. Narrator:**

Rádiu Kultura kinawalenga wasikilizaji wa kituo Praia fm lakini kwa kuzingatia zaidi masuala ya utamaduni.Kinawalenga wasikilizaji wanaopenda miziki, habari na vipindi vya kitamaduni. Rádiu Kultura pia hupeperusha matangazao ya shirika la utangazani la Deutsche Welle kwa Lugha ya Kireno kutoka nchini Ujerumani kwani mshirika mkubwa wa shirika hili la utangazaji.

Lakini Giordano Custodio hakukomea hapo, baada ya kufungua kituo cha pili cha Redio, aliingilia fani ya matangazo ya Televisheni.

**14. SFX STV**

**15. Narrator:**

Kituo cha Televisheni cha STV – Sistema Terra Verde – , ndio mradi wa hivi punde kabisa wa kampuni ya CG Comunicações,kituo kinacholipiwa.Na matangazo yake hasa muziki wakati wa kipindi cha majaribio yalidhihirisha kuwa ni kituo bora zaidi tangu kizinduliwe kati kati mwa mwaka wa 2010.Kituo hiki hupeperusha matangazo yake masaa 24,studio ndogo zilizoko makao makuu ya kampuni ya GC Comunicações. Kituo hiki kimeanzisha matangazo hayo wakati ambapo vituo vingi vya Televisheni havitoi huduma zake kwa muda huo wa masaa 24.

**16. Giordano Custódio:**

"Tulianzisha kituo hiki cha Televisheni kwasababu tuliona soko na mahitaji ya matangazo ya Televisheni yanazidi kuongezeka. Na bado hakuna kituo kilichoweza kutimiza mahitaji haya. Watu hupendelea matangazo bora, na hawajali matangazo hayo yanatoka kituo gani. Ndio sababu kila upitako kote mjini utakuwa milingoti ya kunasa mawasiliano ya Televisheni."

**17. Narrator:**

Kampunii ya GC Comunicações ilianzishwa mwaka wa 1997 ikiwa na wafanyi kazi watatu pekee ambao pia walikuwa washirika wakuu wa kampuni hii, na sasa imeimarika kufika kiwango cha kuwaajri wafanyi kazi 27 katika stesheni hizi za Redio na Televisheni.

Kampuni hiyo sasa inauwezo wa kuleta pato la hadi kima cha Euro 300.000 kulingana na hesabu a hara haaka ya Giordano Custódio. Na pesa hizi hasa hutumika kwa utafiti wa kupanua soko na kuimarisha matangazo.

**18. Giordano Custódio:**

"Kwanza tulifanya utafiti wa kituo cha Redio. Na katika utaiti huo tulichunguza kwa makini masuala yote yanayohusiana na shughuli za utangazaji, tulihakikisha kuwa tunakuwa makini zaidi katika shughuli hii kwani hatukuwa na hakika yaakayotokea badaye.Mbali na hayo pia sisi hufanya utafiti ili kufahamu vyema mahitaji ya wasikilizaji, lugha na vipindi wanavyopenda kusikiliza kupitia vituo vyetu. Hiyo ndio njia pekee ya kufahamu vyema mahitaji ya wasikilizaji wako."

**19. Narrator:**

Vijana wanaotaka kuiga mfano wake lazima wawe na ujasiri na kufungua macho,sio kuvaa miwani ya kuzuia miale ya jua unapoingia katika fani hii, anashauri Giordano Custódio:

**20. Giordano Custódio:**

"Nilikuwa nikisema kuwa huwezi kuanzisha kampuni ukiwa umefunga macho au kuvaa miwani ya kuzuia miale ya Jua kwani kwa kufanya hivyo hutaweza kuona ukweli wa mambo. Jambo la kwanza ni kufanya utafiti wa kuendeleza wazo lako,na pia utafiti wa soko. Usijaribu kuanzisha biashara yoyote bila ya kufanya mambo hayo!"

**21. Narrator:**

Mbali na kufahamu vyema mahitaji ya soko, jambo lingine muhimu ni kuwa na msimamo na kujiamini kwa kila jambo unalolifanya, usiwe mtu wa kuregarega anasema Giordano Custodio

**22. Giordano Custódio:**

"Hapa Barani Afrika wengi wa wafanyi biashara hutaka kujaribu mambo ambayo tayari yamefaulu kwa wengine. Lakini mimi nimeamua kujaribu mambo mapya kila ninapopata fursa hiyo.Yaaani wakati watu wanakwenda Kazkazini mimi hutaka kwenda Kusini, kwani kwa kufanya hivyo, utakutana na watu wenye mahitaji mengi sana kwa shughuli unazofanya upande wa kusini kuliko kasikazini ambako kila mmoja anaelekea."

**23. Narrator:**

Na wakati anapokabiliwa na changamoto nyingi, au matatizo mengi, Giordano Custódio ana mbinu za kujiliwaza ili kujikwamua katika hali hiyo anasema.

**24. Giordano Custódio:**

“Ninapokuwa nimechoka au kufadhaika, mimi hujipumzisha. Usingizi ndio dawa ya mfadhaiko wangu. Ninapo lala kwa muda, huamka nikiwa mchangamfu na kuendelea na kazi.

**25. Narrator:**

Giordano Custódio ni Mtu  mwenye shughuli nyingi sana, kwani ndie msimamizi wa kituo cha Redio na Televisheni mbali na kuandaa vipindi vya Televisheni. Lakini hakosi kutenga muda wa kuwa na famila yake, marafiki na michezo.

**26. Giordano Custódio:**

“Lazime utenge muda wakuwa na Familia yako kwani hii ni muhimu sana. Ninamarafiki pia ambao mara nyingi humaliza kazi zao mwendo wa  saa nne, au tano usiku. Siku yangu huanza saa kumi na mbili asubuhi ambapo huondoka nyumbani na familia yangu. Na pia hutenga muda wa masaa mawili wakati wa chakula cha mchana kuwa na familia yangu.Kuna wakati mwengine huwa nataka kuwa peke yangu na hapo huenda kuogelea baharini na kufanya mazoezi. Yaani kuna muda wa kufanya kila kitu.

**Outro:**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala hii ambapo tumemuangazia Giordano Custódio, mmiliki wa kampuni ya Utangazaji ya GC Comunicações iliypoko mjini Praia, kisiwani Cape Verde. Makala hii imeandikwa na Nélio dos Santos na Johannes Beck. Hiki ni miongoni mwa mfululizo wa vipindi vya Learning-by-Ear- kuhusu wajasirimali wanaofanya vyema Barani Afrika. Endapo ungependa kusikiliza tena kipindi hiki, au kutuma maoni, usisite kutembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.